**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**664** **MITAALA NA UFUNDISHAJI**

**Muda: Saa 3.** **Wednesday, 11th Mei 2011**

---

**Maelekezo.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka sehemu **B** na swali **moja (1)** kutoka sehemu **C**.
3. Sehemu **A** ina alama 36, sehemu **B** ina alama 40 na sehemu **C** ina alama 24.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (alama 36)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Fafanua dhana ya mtaala wa ziada.
2. Orodhesha vipengele vinne (4) vinavyopaswa kujumuishwa katika tathmini ya somo katika andalio.
3. Taja mbinu tatu (3) za kufundishia zinazolingana na mahitaji ya wanafunzi wenye umri mdogo.
4. Kwa nini lengo la jumla la mtaala lina umuhimu kwa mwalimu?
5. Fafanua maana ya Mbinu ya Maonyesho.
6. Taja vigezo vinne (4) vya kupanga maudhui ya somo katika azimio la kazi.
7. Tofautisha maandalizi ya mwalimu na maandalizi ya mwanafunzi katika ufundishaji na ujifunzaji.
8. Eleza umuhimu wa malengo ya utendaji katika ufundishaji.
9. Orodhesha hatua tatu (3) za kuhakiki mazoezi ya kufundishia ya muda mrefu.

**SEHEMU B (alama 40)**

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

10. Jadili namna azimio la kazi linavyosaidia kuzingatia usawa katika utoaji wa maudhui ya masomo.
11. Fafanua faida tano (5) za kupanga maswali ya mtihani kwa kuzingatia viwango tofauti vya uelewa.
12. Chagua somo moja la sanaa au ufundi, kisha andika orodha ya zana za kufundishia na kujifunzia ambazo mwalimu na wanafunzi wanaweza kuzitengeneza wenyewe.
13. Eleza kwa kina jinsi mafunzo ya vitendo yanavyomsaidia mwalimu mwanafunzi kuunganisha nadharia na vitendo vya kufundishia.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU C (alama 24)**

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

14. Jadili mikakati mitano (5) anayoweza kutumia mwalimu kufanya somo lisisimue na kuwavutia wanafunzi wasio na motisha darasani.

15. Eleza umuhimu wa kuzingatia rasilimali zinazopatikana katika kuchagua na kutengeneza zana za kufundishia.

16. Fafanua umuhimu wa maoni ya wadau katika mchakato wa ukuzaji wa mitaala.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org